


## Je! INTRAN nini?

Hii ni huduma ya **bure** na ya **siri**. Tunawatoa wakalimani wa Lugha ya Ishara ya Briteni, wakalimani wa kusoma midomo na wakalimani wa lugha za kigeni kwa lugha 150.

### Kazi ya mkalimani

- Wakalimani wote wa INTRAN ni wataalamu, wamepokea mafunzo ya kitaalamu na wote wamekaguliwa na polisi.
- Wakalimani hukuruhusu wewe na mmoja wa wafanyikazi kuzungumziana.
- Wakalimani hawawajibiki kwa yale yanayosemwa na wafanyikazi. Kama huelewi kinachosemwa, tafadhali sema.
- Wakalimani hawatoj ushauri, lakini wako hapo ili kukusaidia kuongea na mmoja wa wafanyikazi.
- Kila kitu kinachojadiliwa katika mkutano kitashughulikiwa kama cha siri.

## Je, INTRAN inapatikana wapi?

Mahali popote unapoona ishara ya  katika maeneo ya mapokezi ya umma, mtu ataweza kukusaidia kwa lugha yako.

Kwa mfano, hapa kuna baadhi ya huduma ambazo zinaweza kuongea na wewe kupitia mkalimani:

- Madaktari
- Mafamasia
- Makao
- Shule
- Polisi
- Hospitali
- Huduma za Jamii
- Maktaba

Kwa huduma zingine, kama huna uhakika kama INTRAN inapatikana, tafadhali onyesha kadi yako ya INTRAN au uliza mfanyikazi kama unaweza kupata mkalimani.

## Kama unahitaji kutumia INTRAN hivi ndivyo unastahili kufanya

- Mwambie mmoja wa wafanyikazi lugha unayoongea
- Au
- Onyesha kadi yako ya INTRAN
- Au
- Utaonyeshwa kadi/tangazo ambalo unaweza kuonyesha lugha unayoongea
- Kisha
- Subiri wakati wanapompigia mkalimani.
  - Fafanua unachohitaji kwa mkalimani kwa simu.
  - Kama unahitaji kiasi kidogo cha habari hii inaweza kufafanuliwa kupitia mkalimani wa simu.
  - Kama unahitaji miadi utapewa tarehe na wakati. Mkalimani atapatikana kwa miadi yako, mara kwa mara wa uso kwa uso lakini wakati mwingine kwa simu.

